



KENYA REVENUE
AUTHORITY



Mradi wa **Kujitolea**
Kutoa Taarifa
Kuhusu Ushuru

Ni nini Mradi wa Kujitolea Kutoa Taarifa Kuhusu Ushuru?

Huu ni mradi ambao mlipaji ushuru hutoa habari kwa siri kuhusu madeni yake ya ushuru ambayo awali yalifichwa kwa Kamishna kwa lengo la kupunguziwa kulipa penalti na riba ya ushuru uliotolewa taarifa.

Ni ushuru gani unaotozwa kupitia Mradi wa Kujitolea Kutoa Taarifa Kuhusu Ushuru?

Ushuru wa mtu binafsi, Ushuru wa Mashirika, Ushuru wa Malipo kutokana na kiwango cha mapato, asilimia ya ushuru kutoka kwa mtu binafsi au mashirika unaolipwa moja kwa moja kwa serikali, ushuru unaolipwa moja kwa moja kwa serikali kutokana na faida, Ushuru unaotozwa bidhaa inaponunuliwa na mteja, Withholding VAT, ushuru unaotozwa bidhaa au huduma maalum, ushuru unaotozwa jumla ya mauzo katika kipindi maalum, & ushuru unaotokana na kodi ya nyumba kila mwezi.

Utaanza kutumika lini Mradi wa Kujitolea Kutoa Taarifa Kuhusu Ushuru?

Mradi wa Kujitolea Kutoa Taarifa Kuhusu Ushuru utaanza kutumika tarehe mosi Januari 2021 kwa kipindi cha miaka mitatu hadi tarehe 31 Disemba 2023.

Ni vipindi gani vya ushuru vitahusisha Mradi wa Kujitolea Kutoa Taarifa Kuhusu Ushuru?

Kipindi stahiki cha utoaji taarifa kuhusu ushuru chini ya mradi huu kitakuwa ni cha hadi miaka 5 kabla ya tarehe 1 Julai 2020. Hii ni kuanzia tarehe 1 Julai 2015 hadi 30 Juni 2020.

Mtu atatuma vipi ombi la Mradi wa Kujitolea Kutoa Taarifa Kuhusu Ushuru?

Mtu anayetaka kufaidika na Mradi wa Kujitolea Kutoa Taarifa Kuhusu Ushuru atatuma maombi katika mtandao wa iTax katika mapato maalum yaliyotengwa kwa ushuru unaotakikana kulipwa. Maombi yanapokamilika kutumwa, mtu atapokea kikaratasi/ujumbe wa kuthibitisha kupokelewa maombi.

Mtu anayetaka kutuma maombi aingie katika mtandao wa KRA kwa mchakato wa hatua kwa hatua.

Anayetuma maombi atapunguziwa nini katika penalti na riba?

- Ikiwa maombi yamekubaliwa, mlipaji ushuru ataondolewa riba na penalti inayotakikana kulipwa kutokana na deni la ushuru kama ifuatavyo:
- Asilimia 100% itaondolewa ikiwa taarifa imetolewa na deni la ushuru kulipwa katika mwaka wa kwanza wa mradi
- Asilimia 50% itaondolewa ikiwa taarifa imetolewa na deni la ushuru kulipwa katika mwaka wa pili wa mradi
- Asilimia 25% itaondolewa ikiwa taarifa imetolewa na deni la ushuru kulipwa katika mwaka wa mwisho wa mradi.

Je, mtoaji ushuru anaweza kushtakiwa baada ya kutoa taarifa?

Hapana. Mtu aliyepata afueni wa Mradi wa Kujitolea Kutoa Taarifa Kuhusu Ushuru hatoshtakiwa kutokana na madeni yake ya ushuru yaliyopita. Hata hivyo, ikiwa mwombaji ameshindwa kutoa taarifa ya kweli kuhusu madeni yaliyopita ya ushuru, Kamishna anaweza kuondoa afueni, akadirie nyongeza katika ushuru, au aanze mashtaka.

Je, mtu atatarajiwa kulipa kwa mkupuo mmoja?

Kamishna atawekeana mkataba na mtoaji ushuru ambao unafafanua masharti ya malipo ya deni la ushuru. Deni hili la ushuru litalipwa katika kipindi cha mwaka mmoja.

Je, mtu anaweza kujaza faili lilorekebishwa la Mradi wa Kujitolea Kutoa Taarifa Kuhusu Ushuru?

Marekebisho ya faili asilia la Mradi wa Kujitolea Kutoa Taarifa Kuhusu Ushuru yanaweza kufanyika mara moja wakati wowote katika kipindi cha malipo ya mradi huu walichokubaliana, ila tu, marekebisho yasisababishwe mtoa ushuru kuregeshewa malipo ya ushuru ambayo ameshayalipa katika mradi huu.

Je, Mradi wa Kujitolea Kutoa Taarifa Kuhusu Ushuru unahusisha watoa ushuru wote?

Mtoa ushuru hatohusishwa na Mradi wa Kujitolea Kutoa Taarifa Kuhusu Ushuru ikiwa:- i. yuko katika ukaguzi au uchunguzi wa kutotoa taarifa kuhusu ushuru au amepewa notisi kwa lengo la kuchunguzwa au kufanyiwa ukaguzi/iwapo ametimiza masharti ya kutoa taarifa kuhusu ushuru ambao taarifa yake ilikuwa imefichwa, au ii. amechukuliwa hatua za kisheria kutokana na madeni ya ushuru au mas'ala yoyote yanayohusiana na madeni ya ushuru.

Ni masharti gani mengine ambayo yameambatanishwa na Mradi wa Kujitolea Kutoa Taarifa Kuhusu Ushuru?

- Mradi wa Kujitolea Kutoa Taarifa Kuhusu Ushuru unatumika tu, katika kutoa habari kuhusu malipo ya ushuru. Mtu hatopewa afueni ya ushuru itakayosababisha kuregeshewa ushuru aliolipa katika au baada ya kipindi cha Mradi wa Kujitolea Kutoa Taarifa Kuhusu Ushuru au pengine kusababisha kuongezeka kwa deni la ushuru au hasara kupelekwa mbele.
- Mtu aliyepewa afueni katika mradi huu hatoshtakiwa kwa taarifa ya ukweli aliyotoa kuhusu ushuru na ushuru uliolipwa.
- Mtu aliyepewa afueni kuambatana na matakwa ya Mradi wa Kujitolea Kutoa Taarifa Kuhusu Ushuru hawezi kukata rufaa au A person granted relief in accordance with the provisions of the VTDP shall not appeal or seek any other remedy with respect to the taxes, penalties and interest remitted by the Commissioner.

Nini manufaa ya Mradi wa Kujitolea Kutoa Taarifa Kuhusu Ushuru?

- Mradi utatoa nafasi kwa watoaji ushuru ambao awali hawakutoa taarifa kuhusu mapato yao kufanya hivyo bila ya kulazimishwa kulipa penalti na riba. Unanuia kuimarisha ukusanyanyaji wa ushuru kwa kuwafanya watu wengi ambao walikuwa katika shughuli za uchumi zilizojificha kufikika na kulipa ushuru.

Je, mtu atapewa cheti?

- Mtu atapewa cheti cha Mradi wa Kujitolea Kutoa Taarifa Kuhusu Ushuru, ambacho ni thibitisho kuwa mtu alinufaika na mradi huu katika kipindi maalum cha ushuru kilichoonyeshwa na cheti hicho. Cheti kilichotolewa kitahusu tu, ushuru uliotolewa taarifa na vipindi vya ushuru vilivyofanana.



Tel: +254 (020) 4 999 999, +254 (0711) 099 999 | Email: callcentre@kra.go.ke



www.kra.go.ke



@KRACare



Kenya Revenue Authority



Kenya Revenue Authority

Tulipe Ushuru, Tujitegemee!